TANESCO MTANDAONI

Toleo namba 20

Jarida la Mtandaoni | Mei 07, 2024



# MGAO WA UMEME NCHINI SASA UMEKWISHA

**MHE. KASSIM MAJALIWA**



# MGAO WA UMEME NCHINI SASA UMEKWISHA

Mhe. Kassim Majaliwa

## Na Charles Kombe, Dodoma

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amesema kuwa upatikanaji wa umeme nchini umeimarika kwa kiasi kikubwa na kuondoa adha ya mgao wa umeme iliyokuwa ikikwamisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuleta kero kwa wananchi.

Mhe. Majaliwa ameyasema hayo Aprili 19 wakati wa hafla ya kufunga maonesho ya wiki ya nishati katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma baada ya kutembelea maonesho hayo na kupata maelezo ya hali ya upatikanaji wa umeme nchini kutoka kwa wataalam kutoka TANESCO.

> **Wizara yetu ya nishati kupitia TANESCO imemudu kuzalisha umeme mwingi kuliko mahitaji. Mradi wetu mkubwa wa Bwawa la Julius Nyerere ambao unaendelea kukamilika na tumeshaanza kuona matokeo yake ambapo megawati 235 tayari ziko kwenye mfumo na tunaendelea kuzitumia na ndizo ambazo zimetupunguzia sana mgao**
>
> - Mhe. Kassim Majaliwa

Kwa upande wake Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko amesifu utendaji wa Shirika.




> **Watu hawa wanafanya kazi kubwa sana, ni bahati mbaya kuna mazingira fulani yanawasukuma kuwa kwenye eneo ambalo hata wao hawana chakufanya na kwa hiyo brand (taswira) yao wakati mwingine inaonekana tofauti. Na kuna watu ambao wanaamini TANESCO ni wakata umeme. Tunafanya kazi kubwa ya kurekebisha hiyo hali kwa maelekezo yenu**
>
> - Mhe. Dkt. Doto Biteko

Aidha, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Tulia Ackson** amsema sekta ya nishati ni eneo muhimu katika uchumi wa nchi na lengo la Serikali ni kuhakikisha sekta hii inaleta maendeleo.

> **Kwa taarifa zilizotolewa na TANESCO kuhusu gridi tumeona umeme wakutosha unazalishwa. Sasa ili tuwe na uwekezaji wenye tija hatutaki tuwe na umeme sio tu wakuwasha taa na kuchaji simu nyumbani, tunataraji viwanda pia viweze kuwa vingi**
>
> - Mhe. Dkt. Tulia Ackson

Maonesho ya wiki ya nishati Bungeni Dodoma yaliyofanyika kwa siku tano yamefungwa leo Aprili 19 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Kassim Majaliwa.**

# MATUKIO KATIKA PICHA




Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akitazama katika runinga kiwango cha umeme unaozalishwa na namna unavyosafirishwa kulingana na mahitaji



**Mhe. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa** akiwa pamoja na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati **Mhe. Dkt. Dotto Biteko** wakitazama makala maalumu inayoelezea utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya wizara ya nishati




# TANESCO MNAFANYA KAZI NZURI

Mhe. Dotto Biteko

**Na Charles Kombe, Dodoma**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amelipongeza shirika la Umeme Nchini ,TANESCO kwa kuendelea kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha Wananchi wanapata nishati ya umeme.

Mhe. Dkt. Doto Biteko ameyasema hayo Aprili 16, 2024 wakati akifungua maonesho ya wiki ya Nishati katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma

> **TANESCO nawapongeza sana siku hii ya maonesho, mnafanya kazi kubwa endeleeni na moyo huo, akitokea mtu anawarudisha nyuma, kwa utaratibu wenu wa ndani mwambieni usiturudishe nyuma**
>
> **- Mhe. Dkt. Doto Biteko**

Mhe. Dkt. Doto Biteko pia ameeleza namna ambavyo TANESCO imeendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kutoa huduma kwa wananchi.

> **Wakati huu wa mvua nyingi, zilizosababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali Nchini, Nguzo nyingi sana zinaanguka, TANESCO wanafanya kazi kubwa sana kurudisha miundombinu ya umeme kuwa katika hali ya kawaida, Kuna mahali ambapo hata njia ya kufikisha nguzo haipo lakini wanapeba nguzo zile hata kwa matoroli ya punda ili watu waweze kupata umeme**
>
> **- Mhe. Dkt. Doto Biteko**

Naye Naibu Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mussa Zungu amempongeza Naibu Waziri mkuu na Waziri wa nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko kwa kuthibiti changamoto za upatikanaji wa umeme nchini.

> **Kwa sasa umeme tunauona kwa ukamilifu mkubwa sana, 'group' ya wateja ya kulalamikia umeme sasa hivi mengi hayana wachangiaji kwa sababu umeme upo tofauti na mwaka uliopita, sasa hatuoni malalamiko yale**
>
> **- Mhe. Zungu**

> **Mimi ni moja kati ya wabunge niliokuwa nikikusumbua sumbua sana katika masuala ya nishati. Natamka kwamba kuanzia leo sikusumbui tena kwa sababu nimejionea mimi mwenyewe, nina macho ninaona na nina masikio nasikia kwamba Tanzania tuliyokuwa nayo miaka mitatu iliyopita sio Tanzania ya sasa hivi katika masuala ya nishati**
>
> **- Mhe. Zungu**

Nae mbunge wa Kinondoni Mhe. Abass Tarimba amesema awali alikuwa anapata changamoto kubwa katika suala la umeme kwa wananchi wake lakini kwa sasa hali imebadilika.

**Mimi ni moja kati ya wabunge niliokuwa nikikusumbua sumbua sana katika maswala ya nishati. Natamka kwamba kuanzia leo sikusumbui tena kwa sababu nimejionea mimi mwenyewe, nina macho ninaona na nina masikio nasikia kwamba Tanzania tuliyokuwa nayo miaka mitatu iliyopita sio Tanzania ya sasa hivi katika masuala ya nishati**

**- Mhe. Tarimba**

**Maonesho ya wiki ya nishati yaliyofanyika Bungeni jijini Dodoma tarehe 15 Aprili mpaka tarehe 19 Aprili 2024 ambapo Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Nishati zimeshiriki katika maonesho hayo, lengo kuu likiwa ni kuleta mrejesho kwa wabunge juu ya masuala mbalimbali yanayohusu Wizara ya Nishati ikiwemo majibu ya changamoto za Umeme katika majimbo yao na mrejesho wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali.**




# WAAJIRI WAPENI WAAJIRIWA VYOTE VINAVYOSTAHILI KULINDA USALAMA WAO KAZINI

Mhe. Dkt. Doto Biteko

**Na. Agnes Njaala, Njiro Arusha**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya usalama na afya kazini yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya Njiro jijini Arusha, amewataka waajiri kuhakikisha wanawapa waajiriwa mahitaji yote wanayostahili ili kulinda usalama wao katika utendaji wa kazi katika mazingira yote

Mhe. Dkt. Doto Biteko amebainisha kuwa mfanyakazi anapokuwa salama mahala pa kazi inampa amani na furaha na inachangia kumfanya awe na utendaji mzuri wenye tija utakaoongeza uzalishaji sambamba na kupunguza gharama za uzalishaji kwa mwajiri.

> **Waajiri na waajiriwa hakikisheni mnazingatia usalama mahali pa kazi, mtu wa kwanza kujali usalama wake ni mwajiriwa, ukiona mtambo hauko salama toa taarifa kwa mwajiri wako hapa hautaonekana umegoma bali ni kuhakikisha mazingira ya kazi yanakuwa salama**
>
> **- Mhe. Dkt. Doto Biteko**

Aliendelea kwa kusema kuwa, kila mwajiriwa katika eneo lake ahakikishe kuwa utendaji wake unachangia katika uzalishaji ili kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kuhakikisha anakuwa mstari wa mbele katika kulinda usalama wake awapo kazini

> **Ni vyema kwa kila mtumishi kujidhatiti katika kuhakikisha anafanya kazi kwa kuzingatia misingi na mikakati iliyowekwa katika mazingira salama kwani ni dhahiri kuwa hakuna atakaye jenga uchumi wa nchi yetu isipokuwa sisi wenyewe**
>
> - Mhe. Dkt. Doto Biteko

Aidha, amewataka Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) kuepuka vitisho wakati wa utekelezaji wa majukumu yao na badala yake wajenge uhusiano bora na waajiri pamoja na waajiriwa ili kuwezesha lengo la kupeana elimu bila vikwazo.

> **Niwatake OSHA kuondoa vitisho wakati mnapowafata waajiri na waajiriwa wekeni mahusiano mazuri nao ili wawaone ni kimbilio pale wanapowahitaji**
>
> **- Mhe. Dkt. Doto Biteko**



**Akihitimisha hotuba yake Mhe Biteko amesisitiza umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo husababisha hasara kote duniani kwa kuleta athari kwa wananchi na mali zao na zaidi kuathiri nguvu kazi hali ambayo hupelekea uchumi wa nchi kuyumba.**

**Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO ) ni moja kati ya taasisi za serikali ambazo zimeshiriki maonesho hayo ya kitaifa ya OSHA yaliyoanza Aprili 24,2024 ambapo imepata nafasi ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na ajali za umeme ili kuepukana na athari za mali zao, vifo pamoja na ulemavu wa kudumu.**





## TUTAENDELEA KUTATUA CHANGAMOTO ZA MASLAHI KWA WAFANYAKAZI ILI TANESCO IWE SEHEMU BORA KUFANYA KAZI

Mha. Athanasius Nangali

**Na. Agnes Njaala, Mount Meru Arusha**

Kila mwaka hufanyika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi (Mei Mosi) duniani kote, mwaka huu 2024 maadhimisho hayo yamefanyika kitaifa mkoa wa Arusha ambapo kama Shirika tulipata nafasi ya kushiriki kwenye maadhimisho na maonyesho huku tukionesha umma maboresho ya huduma zetu ambayo yamefanywa na Shirika.

Maadhimisho hayo ya Mei Mosi yalienda sambamba na sherehe ya jioni ya kuwapongeza wafanyakazi bora taifa iliyofanyika katika ukumbi wa Mount Meru jijini Arusha ikiongozwa na mgeni rasmi ambaye ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usambazaji Mha. Athanasius Nangali akimuwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika letu Mha. Gissima Nyamo-Hanga.

Akizungumza na wafanyakazi wakati wa hafla hiyo, Mha. Nangali amesema kuwa uongozi wa Shirika unaendelea na kila juhudi za kutatua changamoto za maslahi kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa kikamilifu maslahi yao husika ili kuifanya TANESCO kuwa mahali sahihi kufanya kazi hatua inayolenga kuongeza ari na kuinua utendaji wa kazi kwa manufaa ya Shirika na nchi kwa ujumla.

> Kwa kweli uongozi umepiga hatua kama mlivyoshuhudia maboresho kadhaa katika sikukuu ya Krismasi na Idd el Fitri ambapo tumeweza kuwashika mkono wafanyakazi na pia upande wa Bima ya Afya kifurushi kimerudishwa na hapohapo baadhi yenu tayari wamewekwa kwenye madaraja yao stahiki
>
> \- Mha. Athanasius Nangali

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Rasilimali Watu na Utawala Bi. Magreth Mwandu amewahakikishia wafanyakazi kuwa uongozi unawapenda na kuwathamini na unatambua michango ya kila mmoja hivyo ifahamike kuwa Menejimenti ya Shirika ipo pamoja na wafanyakazi wote katika hali zote kuwalinda na kuwawekea mazingira na hali bora katika kutekeleza majukumu ya Shirika.

Naye kaimu Mwenyekiti TUICO taifa Bi. Janeth Vesso, amewapongeza wafanyakazi wote na kuwaasa wafanyakazi bora taifa kuwa wasibweteke kwakuwa wameibuka washindi bali waendeleze kujituma na kuwa na bidii ya kazi ili kutendea haki ushindi walioupata.

> **Niwatake wafanyakazi wote kuendeleza kufanya kazi kwa uaminifu, bidii na uweledi ili tujenge taswira nzuri ya Shirika letu na hatimaye kulitoa hapa lilipo kulifanya liwe Shirika bora Afrika**
>
> **- Bi. Janeth**

Akitoa salamu za shukrani mfanyakazi bora taifa Mhandisi Moses Holela ambaye ni Meneja wa kituo cha kufua umeme cha Mtera amesema kuwa, anashukuru kwa kuchaguliwa kuwa mshindi wa kwanza na amepokea kwa furaha ushindi huo.

**Nina furaha kubwa kuibuka mshindi wa kwanza nipende kutoa rai kwa wafanyakazi wenzangu kote nchini kuendeleza juhudi za kufanya kazi kwa bidii, weledi na maarifa kwani jitihada za kila mfanyakazi uonekana popote alipo kama ambavyo imeonekana kwangu**

**- Mha. Holela**

## MATUKIO KATIKA PICHA




**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika Mha. Athanasius Nangali akimkabidhi mfanyakazi bora taifa kwa mwaka 2024 Mha. Moses Holela zawadi ya Televisheni**





**Kundi la Wanamichezo wakikabidhi vikombe vya ushindi kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika Mha. Athanasius Nangali wakati wa halfa ya Mei Mosi 2024 Mount Meru Hotel jijini Arusha.**




Baadhi ya Washiriki wa maonesho ya usalama na afya kazini yaliyofanyika kitaifa Aprili 24 hadi 30, 2024 katika viwanja vya Njiro jijini Arusha, wakikabidhi kwa kaimu Mkurugenzi Mtendaji Mha. Athanasius Nangali tuzo ya ushindi wa pili katika Sekta ya Nishati




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika Mha. Athanasius Nangali akikabidhi keki kwa kamati ya maandalizi ya sherehe ya Mei mosi 2024






# MKOA WA MANYARA WATOA MSHINDI WA NNE KITAIFA MEI MOSI 2024

**Na. Kelvin Kasambala, Manyara**

Siku ya Mei Mosi 2024 Mkoa wa Manyara waliadhimisha sikukuu hio tarehe 29 Aprili 2024 katika uwanja wa Kwaraa Babati.

Katika siku hiyo TANESCO Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Meneja wa Mkoa pamoja na wafanyakazi wote waliadhimisha siku hiyo kwa kuonyesha uhodari wa kuwatumikia wananchi wa Mkoa wa Manyara sambamba na mikakati ambayo Mkoa imefanikiwa kuitumia katika kuboresha huduma kwa wateja na mbinu mpya ambazo Mkoa umepanga kuzitumia kwa lengo kuu la kuhakikisha wananchi wa Manyara wanapata huduma.

Mgeni rasmi katika siku hiyo ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa ndugu Lazaro alipata fursa ya kutembelea banda la TANESCO na kupata maelezo yote sambamba na vitabu maalum vilivyoandaliwa vinavyoonyesha miradi yote ya umeme, utekelezaji wa miradi hadi kufikia Aprili 2024, maeneo ambayo hayana huduma sambasamba na gharama halisi.

Baada ya maadhimisho hayo, wafanyakazi wote kwa pamoja walishiriki chakula cha mchana na kukata keki kuonyesha ushirikiano kwa wana Manyara na baadae kurejea ofisini kwa ajili ya kuendelea kuwahudumia wateja.

Hata hivyo jitihada zote ziliweza kufanikiwa kikamilifu chini ya usimamizi hodari kwa Mhandisi Jahulula Maendeleo Jahulula ambaye ni Meneja wa Mkoa, hii iliweza kudhibitishwa kuanzia ngazi ya Mkoa kwa kuwa mfanyakazi bora wa Mkoa kwa mwaka 2024 hadi ngazi ya kitaifa kwa kushika nafasi ya 4 kitaifa akipeperusha bendera ya Mkoa wa Manyara.

Washindi wengine ambao walipewa zawadi ni Bi. Vivian Kadele ambaye ni Mhasibu kutoka ofisi ya Katesh na Bi. Agness Momoya ambaye ni Fundi kutoka ofisi ya Mbulu ambapo wote walipewa zawadi.



## MATUKIO KATIKA PICHA




Mshindi wa nne kitaifa **Mha. Jahulula Jahulula** (Mwenye suti nyeusi) akiwa na baadhi ya wafanyakazi wa Manyara katika hafla ya kuwapongeza wafanyakazi bora jijini Arusha.






# MKUU WA MKOA WA LINDI AMEWATAKA WAFANYAKAZI WA TANESCO KUFANYA KAZI KWA BIDII KWA MASLAHI MAPANA YA TAIFA

**Na. Fredy Mbavai, Lindi**

Wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Lindi waliungana pamoja na wafanyakazi wote duniani katika maadhimisho ya Mei Mosi 2024, yaliyofanyika katika uwanja wa shule ya msingi Likangara Wilaya ya Ruangwa.

Katika maadhimisho hayo mgeni rasmi  Mhe. Mkuu wa Mkoa Lindi Zainab Talek amewataka wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii,ubunifu na uweledi kwa maslahi mapana ya Taifa.

> **Napenda mfahamu kuwa Serekali inatambua mchango mkubwa kutoka kwa Mashirika ya umma na yasio yakiserikali katika kujenga uchumi wa taifa letu hivyo ni vyema mkaendeleza bidii ya kazi ili tusirudi nyuma**
>
> **- Mhe. Talek**

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa **TANESCO** Mkoa  wa Lindi,  Mha.Emmanuel Sengwaji aliwataka wafanyakazi  kuongeza ufanisi katika utendaji kazi ili kupunguza za gharama za uendeshaji kwa Shirika.

Nao wafanyakazi bora walipata nafasi ya kutoa neno la shukrani ambapo katika maelezo yao wameahidi  kutobweteka na badala yake wanaendelea na juhudi za kufanya kazi kwa bidii ili kuleta matokeo zaidi ya kiutendaji kwa Shirika na kulinda imani ya wafanyakazi wenzao ambao wamewapigia kura .



Wafanyakazi TANESCO Lindi washiriki pamoja chakula cha mchana kama ishara ya upendo, mshikamano na umoja (Katika picha wa kwanza ni kaimu Meneja wa Mkoa Mha. Emmanuel Sengwaji)




# FANYENI KAZI KWA MUJIBU WA TARATIBU, KANUNI NA MISINGI YA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA

Mhe. Rosemary Senyamule

## Na. Monica Mabada, Dodoma

Wafanyakazi wa TANESCO Mkoa wa Dodoma pamoja na Makao Makuu wameungana katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi yaani "Mei Mosi"

Sherehe hizo za Mei Mosi zilianza kwa maandamano ya wafanyakazi kuanzia viwanja vya Bunge Dodoma hadi Uwanja wa Jamhuri.

**Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Rosemary S. Senyamule ambapo katika hotuba yake alisisitiza watumishi wa umma kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu, kanuni na misingi ya maadili ya utumishi wa umma ili kutatua kero za wananchi.**

Aidha Mheshimiwa Senyamule, alisema rushwa ni adui wa haki hivyo wafanyakazi wajiepushe na masuala yote ya rushwa na aliagiza hatua kali zichukuliwe kwa watumishi wote watakaojihusisha na rushwa mahali pa kazi.

Mheshimiwa mkuu wa Mkoa aliongezea kuwa wafanyakazi pia tushiriki katika kukemea matukio ya ukatili yanayotokea katika jamii zetu pamoja na kufanya mazoezi ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Mwisho mgeni rasmi aliwaasa wafanyakazi wa Mkoa wa Dodoma kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wa Dodoma kupitia kauli mbiu ya "Kero yako, wajibu wangu.



**Gari lenye kauli mbiu ya siku ya wafanyakazi duniani na pamoja na bango la huduma za Jisoti na Nikonekt likipita mbele ya mgeni rasmi katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani Mei Mosi mkoani Dodoma.**





# TANESCO YAMKABIDHI MKANDARASI UJENZI WA NJIA YA UMEME CHALINZIE - DODOMA

**Na. Shamu Lameck - Pwani**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) limemkabidhi Kampuni ya TBEA ya nchini China Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye urefu wa kilomita 345 kutoka kituo cha Kupokea na kupoza umeme cha Chalinze kuelekea Dodoma.

Akizungumza katika hafla hiyo April 17, 2024 Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mha. Gissima Nyamo-Hanga amesema kwa sasa kituo cha Chalinze kinaweza kubeba megawati 850, hivyo mradi ukikamilika umeme wote kutoka Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere utaweza kusafirishwa kupitia njia hiyo ya chalinze - Dodoma na kufikishwa katika maeneo mengine ya nchini.

> **Mradi huu ni mkubwa una kilometa 345 na gharama yake ni bilioni 510 za kitanzania, sisi kama watumishi tunaowajibu mkubwa wa kuhakikisha tunasimamia rasilimali hii ya Serikali ambayo inawekwa hapa kwa ajili ya watanzania**
>
> **- Mha. Gissima Nyamo-Hanga**

Ameeleza kuwa umeme huo utasafirishwa kupitia njia hiyo kwenda kwenye Kituo cha kupoza umeme cha Zuzu kilichopo jijini Dodoma na kuwa baada ya umeme kufikishwa hapo itakuwa rahisi kufika maeneo mengine ya nchini.

Aidha, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TANESCO, Dkt. Rhimo Nyansaho amesisitiza mradi huo kukamilika kwa wakati huku akiitaka Menejimenti ya TANESCO kusimamia kwa ukaribu zaidi ili kubaini changamoto mapema kama zikitokea.

> **Kutokana na umuhimu wa njia hii ya kutoka chalinze kwenda Dodoma, tumsisitize Mkandarasi kwamba kazi hii inachukua miezi isiyopungua 22, fedha zipo kila kitu kipo tuhakikishe anaweza kumaliza hii kazi ndani ya miezi 22**
>
> **- Dkt. Rhimo Nyansaho**

Ameongeza kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na njia za kusafirisha umeme zenye ubora ili kuwezesha umeme unaozailishwa kwenye vyanzo mbalimbali unakuwa na tija.

> **Tulichokikwepa ni kuwa na maneno mengi mwisho wa siku watanzania wanataka umeme**
>
> **- Dkt. Rhimo Nyansaho**

# MATUKIO KATIKA PICHA




Mkurugenzi Mtendaji TANESCO Mha. Gissima Nyamo-Hanga, akiendesha kikao cha kumkabidhi Mkandarasi mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolti 400 kutoka chalinze kwenda Dodoma.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TANESCO, Dkt. Rhimo Nyansaho akikagua kituo  cha kupokeana kupoza umeme cha Chalinze, kabla ya kumkabidhi Mkandarasi mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolti 400 kutoka chalinze kwenda Dodoma.



# MAFUNDI WA KURUGENZI YA USAFIRISHAJI UMEME, WANOLEWA

**Na. Salama Kasamalu**

Mafundi Sanifu na Mchundo wapatao 20 kutoka Kurugenzi ya Usafirishaji Umeme Aprili 25, 2024 wamehitimu mafunzo ya matengenezo ya njia hai za kusafirisha Umeme (live line) waliyokua yakitolewa kwa muda wa wiki 8, katika Chuo cha Mafunzo Cha TANESCO - TTS Masaki.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Usafirishaji Umeme, Mhandisi Deogratius Mariwa amesema kuwa mafunzo hayo yatawezesha mafundi kufanya matengenezo katika njia za kusafirisha umeme bila kuzimwa kwa njia hizo (live line), na hivyo kutokuathiri hali ya upatikanaji umeme kwa wananchi.

> **Kutokana na mabadiliko ya teknolojia sasa hivi tunafanya matengenezo kwenye njia za kusafirisha umeme zikiwa live kabisa kwa maana kuwa umeme unaendelea kupita, na huku tukifanya kazi, hii yote ni jitihada za kuhakikisha umeme unaendelea kusafirishwa katika njia za kusafirisha umeme na huku tukiendelea na matengenezo ili mwananchi aweze kupata Umeme huu bila kuathiriwa na matengenezo hayo, labda kama kutakua na hitilafu kwenye njia za kusambaza Umeme (Distribution)**
>
> **- Mha. Mariwa**

Aidha ameongeza kwa kusema kuwa mafunzo hayo yamegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 1.8, ambapo jumla ya mafundi 40 watapata mafunzo hayo, kwa awamu 2, na waliohitimu hivi sasa ni mafundi 20 wa awamu ya kwanza.

Naye Meneja wa Mkataba wa mafunzo ya matengenezo katika njia hai za kusafirisha Umeme (live line) Mhandisi Yusuf Salim amesema kuwa TANESCO imeingia mkataba na Kampuni ya EDUBE Electric Consultancy ya Afrika Kusini kwa ajili ya kuwa mkufunzi na kwa asilimia 90 Kampuni ya EDUBE imefikia matarajio ya Shirika kwa kutoa mafunzo madhubuti kwa mafundi hao.

Ameongeza kwa kusema kuwa kupitia mafuzo waliyopata mafundi wameweza kufanya matengenezo katika njia za kusafirisha Umeme za 66Kv-220KV, kwa kuanza na njia ya kusafirisha Umeme ya Dar es salaam-Tanga-Kilimanjaro na lengo likiwa kufanya maboresho katika njia zote za kusafirisha Umeme nchini.

Wahitimu hao wameonesha hali ya kuwa tayari katika kufanya kazi mara watakaporudi katika vituo vyao vya kazi, ambapo walisema kuwa kazi hizo walikua wakizifanya hata kabla ya kupata mafunzo hayo lakini mafunzo waliyoyapata yatawapa uwezo wa kufanya vizuri zaidi alisema mmoja wa wanafunzi hao Bw. Josephat Buyengeza kutoka Mkoa wa Shinyanga

Awamu ya 2 ya mafunzo ya matengenezo katika njia hai za kusafirisha Umeme yanatarajiwa kuanza tena Mei 13, 2024, yatakayohusisha wanafunzi (mafundi) 20 wa idara ya usafirishaji Umeme katika Ofisi za TANESCO Mikoa yote Nchini.


TANESCO
TANESCO YASHINDA KWA KISHINDO
MASHINDANO MEIMOSI 2024
Mshindi wa kwanza Mpira wa Miguu
Mshindi wa pili Volleyball (ke)
Mshindi wa pili draft (me),
Mshindi wa tatu Volleyball (me),
Mshindi wa tatu karata (me).
www.tanesco.co.tz
#TupoKazini


TANESCO
AOSH 2024
1st Runner up
Electricity, Gas, Steam and Air Conditioning Supply
World Day for Safety and Health at Work 2024
Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO ) yatwaa tuzo ya mshindi wa pili katika Sekta ya Uzalishaji Umeme Tanzania, tuzo ambazo zimetolewa Aprili 30,2024 na OSHA wakati wa kufunga maonesho ya kitaifa ya usalama na afya mahala pa kazi yaliyofanyika Njiro jijini Arusha.
www.tanesco.co.tz
#TupoKazini

## BODI YA WAHARIRI

| | |
|---|---|
| 1. Mha. Boniface Gissima Nyamo-Hanga | - Mwenyekiti |
| 2. Irene Gowelle | - Mhariri Mkuu |
| 3. Augustino Kasale | - Mhariri |
| 4. Agnes Njaala | - Mwandishi |
| 5. Salama Kasamalu | - Mwandishi |
| 6. Charles Kombe | - Mwandishi |
| 7. Shamu Lameck | - Mwandishi |
| 8. Kelvin Kasambala | - Mwandishi |
| 9. Fredy Mbavai | - Mwandishi |
| 10. Monica Mabada | - Mwandishi |
| 11. Michael Sokotta | - Mbunifu Kurasa |
| 12. Nurdin Amiri Killo | - Mpiga Picha |
| 13. Thomas Tito | - Mpiga Picha |




TUFUATILIE KUPITIA

**KURASA ZETU ZA MITANDAO YA KIJAMII KUPATA TAARIFA SAHIHI ZA SHIRIKA**

www.tanesco.co.tz